**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

# SHULE YA SEKONDARI BIHAWANA

S.L.P 934, DODOMA Barua pepe:bihawana.sec@dodomacc.go.tz
Simu 1: +255 752 537 613 Simu 2: +255 744 000 220






Tovuti: www.bihawanasecondary.org

Kwa mzazi/mlezi wa: _________________________

Tahasusi ya: _________________Kidato cha Tano 2022/2023

S. L. P _________________, Mji/Wilaya:________________

YAH: **KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BIHAWANA KIDATO CHA TANO (V) MWAKA 2022/2023**

## 1.0 UTANGULIZI.

Shule ya Sekondari Bihawana ni Shule ya bweni inayodahili wanafunzi wavulana wa Kidato cha Tano na Sita tu. Shule inatoa Elimu ya sekondari ya juu (Advanced Secondary Education) katika tahasusi za CBA, CBG, HGL, PCB na PCM. Ilianzishwa na Wamisionari ya Kipashonisti wa Kanisa katoliki mwaka 1961. Mwaka 1974 ilichukuliwa na Serikali ambapo ilianza kuendeshwa na Serikali ya Tanzania; hivyo Shule hii ni miongoni mwa Shule kongwe nchini.

Kwa namna ya pekee kabisa napenda kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari kongwe ya Bihawana kama mwanafunzi wa kidato cha Tano katika mwaka wa masomo 2022/2023. Shule itafunguliwa tarehe ……………., hivyo unatakiwa kuripoti shuleni kwa kipindi cha kuanzia tarehe……………..hadi tarehe………………… Tarehe ya kufungua/kuripoti shuleni inaweza kubadilika kutegemea maagizo ya Mamlaka zenye dhamana.

## 2.0 KUFIKA ILIPO SHULE:

Shule ipo mkoani Dodoma katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma katika barabara kuu ya Iringa. Kuna umbali wa kilometa **18.4** kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma zamani Ofisi za CDA. Ili kufika shuleni ukitokea stendi kuu ya mabasi (Nane nane) panda daladala ziendazo stendi ya daladala ya sabasaba (mjini kati); kisha panda bajaji zinazoenda stendi ya daladala ya kikuyu (stendi mpya) ambapo utazikuta daladala za kuja Shuleni (daladala za Mbabala). Ukipanda daladala ya Mbabala utatakiwa kushuka kituo kijulikanacho kama kibaoni (kibao cha Shule ya Sekondari Bihawana) ambapo utakuwa umefika.

## 3.0 MAMBO MUHIMU YA KUFANYA

Pamoja na kukupongeza kwa kufanikiwa kupata nafasi hii muhimu ya kujiunga na kidato cha Tano, ninatumia fursa hii kusisitiza yafuatayo:-

a) **Kusoma kwa makini** maelezo yote yaliyoko katika fomu hii ya kujiunga (Joining Instructions) na Shule ya Sekondari Bihawana ili kuyatekeleza bila kisingizio. Utekelezaji huo utaleta ufanisi na tija katika kukupatia Elimu iliyo bora kwa muda wote wa masomo Shuleni.

b) Kujaza fomu Na: 1, 2, 3 na 4 na kuzirudisha shuleni wakati wa kuripoti. Fomu na.3 ijazwe na daktari wa hospitali au kituo cha afya cha serikali. Fomu zote zibandikwe picha za 'passport size' kama zinavyoelekeza.
c) Kuzisoma na kuzielewa Sheria za Shule ambazo ndizo ni msingi wa uendeshaji wa Shule.

## 4.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 4.1 Afya

a) Kila mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni akiwa na kadi ya bima ya afya (NHIF) na kama hana atatakiwa kujiunga na mfuko wa bima ya afya na kupata kadi kwa gharama ya **Tsh.52,000.00 kwa mwaka** mara anaporipoti shuleni.
b) Kila mwanafunzi lazima apimwe afya yake kabla ya kujiunga na shule na wakati wowote shule itakapoona kuna haja na umuhimu wa kufanya hivyo.
c) Endapo mwanafunzi ataugua ataomba kibali kwa mwalimu wa zamu/mwalimu mlezi baada ya uthibitisho wa muuguzi wa shule. Baada ya kuruhusiwa atatakiwa kwenda hospitali na kurudi siku hiyo hiyo. Ruhusa ya kulala nje ya shule itatolewa na Mkuu wa Shule.
d) Mwanafunzi mwenye tatizo la kiafya kama vile pumu, moyo, kifua kikuu n.k lazima tatizo lake lithibitishwe na daktari wa hospitali ya serikali ambaye atamshauri mgonjwa na shule kwa maandishi.
e) Kila mwanafunzi anatakiwa kula chakula cha shule mesini au maeneo yaliyoruhusiwa na shule. Hairuhusiwi mwanafunzi kula chakula nje ya maeneo yasiyoruhusiwa kama vile bwenini au darasani.
f) Kila mwanafunzi anapaswa kutunza mwili wake na kuwa safi wakati wote kwa kukata kucha, kuoga, kupiga mswaki, kutandika kitanda na kupanga vitu vizuri bwenini. Hairuhusiwi kuvaa pete, mikufu na mapambo mengine

### 4.2 Sare ya Shule

a) Mashati mawili meupe mawili (02) au zaidi ya mikono mirefu yenye mfuko mmoja. Mashati ya meupe ya tomato yanashauriwa zaidi. Shati lazima lioneshe namba tano ya kirumi **V** kwenye mabega yote mawili (kwa kutumia kitambaa cha suruali) itakayosomeka kwa mbele.
b) Suruali mbili (02) au zaidi za rangi ya **blue nyeusi** (dark blue) zilizoshonwa vizuri zenye marinda mawili na mfuko mmoja wa nyuma usio na zipu na pindo la chini (turnup) la upana wa nchi 18 (suruali zilizobana (modo) hazitaruhusiwa) na mkanda mweusi wa ngozi. Upana wa chini ya suruali utapimwa wakati wa kuripoti.

c) Viatu vya rangi nyeusi vya **kufunga na kamba** na visiwe na visigino virefu pamoja na soksi ndefu nyeupe jozi mbili au zaidi.
d) Nguo za michezo ni Tracksuit ya rangi ya **damu ya mzee/maruni** (yenye mistari myeupe ubavuni) isiyo na maandishi, raba na soksi za blue.
e) Sweta la blue nyeusi (darkblue) la mtindo wa V - shingoni isiyo na mikono (maarufu kama kizibao) yanapatikana shuleni kwa bei ya Tsh.15,000.00 kila moja)
f) Nguo za kushindia ni fulana (Tshirt) mbili (02) au zaidi zenye kola na mikono mifupi rangi ya blue na sizizo na maandishi. Zinapatikana shuleni kwa gharama ya Tshs.15,000.00 kwa kila moja.
g) Raba jozi moja kwa ajili ya michezo.
h) Viatu vya wazi (sandals) kwa ajili ya kushindia. Mwanafunzi hataruhusiwa kuvaa ndala wala yeboyebo. Yeboyebo zitatumika bafuni na maliwato tu.
i) Mzazi unashauriwa kumpatia mwanao mahitaji ya kutosha kwani hataruhusiwa kutoka nje ya shule kwa muda wote wa masomo.

**ZINGATIA:** Nguo ambazo siyo sare ya shule haziruhusiwi shuleni. Ukaguzi wa vifaa/vitu vyote vitakavyoletwa shuleni utafanyika. Ukipatikana na vifaa/nguo zisizohitajika utalazimika kuzirudisha nyumbani. Mwanafunzi aripoti shuleni akiwa amevaa sare.

**MAHITAJI MUHIMU YA BWENI/HOSTEL**

a) Chombo cha kulia chakula na kijiko vinapatikana Shuleni.
b) Ndoo mbili za lita 10 za plastiki kwa kuogea na kufulia na kidumu cha lita 5 cha kuhifadhia maji ya kunywa bweninini.
c) Chupa ya kutunzia maji ya kunywa nje ya bweni.
d) Shuka tatu (02) au zaidi zisizo na maandishi za rangi ya pink na foronya yake na mto.
e) Taulo ya kuogea na mkebe wa kuwekea sabuni yaani 'soap Dish'
f) Chandarua kimoja cha mbu kilichowekwa dawa.
g) Nguo za ndani za kutosha (angalau tano) sio bukta za michezo.
h) Sabuni za kutosha za kuogea na kufulia.
i) Sanduku imara la chuma (tranka) moja tu kwa ajili ya kutunzia nguo, vitabu, n.k.
j) Begi jeusi la kubebea daftari na vitabu. Mwanafunzi hataruhusiwa kutumia mifuko au viroba kubeba vitabu wala daftari.

**ANGALIZO**

a) Mwanafunzi asije na mizigo au begi kubwa shuleni, aje na Tranka moja tu.

b) Hairuhusiwi mwanafunzi kutembelewa na wageni wakati wote atakaokuwepo hapa shuleni ISIPOKUWA kwa wito iwapo italazimika. Siku ya kuwaona wanafunzi ni siku ya mahafali ya kidato cha Sita.

c) Ni muhimu kwa mzazi/mlezi kutoa nafasi kwa walimu kufanya kazi zao bila usumbufu kwa kumshirikisha mwanafunzi mambo yasiyo na tija kwake akiwa shuleni.

## 5.0 ADA NA MICHANGO YA SHULE

a) **Ada ya shule kwa mwaka** ni shilingi 70,000.00. Unaweza kulipa kiasi cha shilingi 35,000.00 kwa muhula au kulipa ada yote mara moja.

b) **Michango**

Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi/mlezi imeorodheshwa katika jedwali hapa chini:

| Na. | Aina ya Mchango | Kiasi | Muda wa malipo |
|---|---|---|---|
| 1 | Ada | 70,000.00 | Kila mwaka |
| 2 | Ukarabati wa Samani | 25,000.00 | Kila mwaka |
| 3 | Kitambulisho | 5,000.00 | Inalipwa mara moja |
| 4 | Taaluma | 30,000.00 | Kila mwaka |
| 5 | Vibarua (wapishi, walinzi) | 30,000.00 | Kila mwaka |
| 6 | Huduma ya Kwanza | 15,000.00 | Kila mwaka |
| 7 | Taahadhari | 10,000.00 | Inalipwa mara moja |
| **JUMLA** | | **185,000.00** | |

Hivyo jumla ya ada na michango kwa kila mwanafunzi ni shilingi **185,000.00** (laki moja na themanini na tano elfu tu). Malipo yote yalipwe kupitia Benki ya NMB tawi lolote au Wakala yeyote nchini kwa kupitia akaunti namba **50501100168** yenye jina la **'Bihawana Secondary School'.** Stakabadhi zote za malipo (bank pay-in-slip) ziletwe Shuleni zikiwa na jina la mwanafunzi, kidato na tahasusi yake nyuma.

**ANGALIZO**: Shule haitahusika na malipo yoyote yatakayofanywa bila kupitia benki.

## 6.0 MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI.

a) Squizer na soft broom kwa wanafunzi wote

b) Dawa ya kufanyia usafi vyooni aina ya CARELINE kwa kila mwanafunzi.
c) Panga kwa wanafunzi wa HGL.
d) Jembe na mpini wake kwa wanafunzi wa CBA na PCM.
e) Fagio ngumu ya kusugulia chooni (hard brush) na fyekeo kwa wanafunzi wa PCB.
f) Shoka na mpini wake kwa wanafunzi wa CBG.
g) Ream mbili za karatasi aina ya A4 kwa kila mwanafunzi kwa mwaka.
h) "Dissection kit" kwa wanafunzi wa CBA, CBG na PCB.
i) Picha (passportsize) nne za hivi karibuni.
j) Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
k) Nakala ya cheti cha kumaliza kidato cha nne (leaving certificate).
l) Hati ya matokeo ya Kidato cha Nne (result Slip).

Aidha kila mwanafunzi anashauriwa kununua vitabu muhimu kwa kila somo analosoma. Vitabu vinavyoshauriwa ni vile vilivyotolewa na Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE).

## 7.0 SHERIA ZA SHULE.

### 7.1 Ratiba ya Shule.

Kila mwanafunzi azingatie kwa makini ratiba ya shule kwa kuwa mahali panapohusika kwa wakati muafaka. Kila mwanafunzi anatakiwa kuamka saa 11:00 asubuhi ili kujiandaa kwa ratiba ya siku. Aidha anatakiwa kufanya yafuatayo: -

a) Kufanya usafi katika eneo lake alilopangiwa (special area)
b) Awahi msitarini (parade) na kuchukuliwa mahudhurio mapema kengele inapogongwa, wachelewaji watashughulikiwa ipasavyo.
c) Kuingia darasani na kuhudhuria vipindi vyote kama vilivyo katika ratiba ya shule.
d) Ni lazima na sio hiari kwa mwanafunzi kufanya mazoezi yote yanayotolewa ndani na nje ya darasa
e) Kutii na kuheshimu kengele kwa kuwa mahali panapohusika kwa wakati mwafaka.

### 7.2 Matumizi ya Sare za Shule

a) Kila mwanafunzi atatakiwa kuwa katika sare ya shule kama ilivyoainishwa katika fomu ya kujiunga na shule (Joining Instruction).
b) Wakati wa michezo wanafunzi wote watakuwa katika sare kamili ya michezo wakati wa ushiriki wao katika michezo na siyo vinginevyo.
c) Wanafunzi wawe na sare kamili wakati wote.
d) Wanafunzi wanaruhusiwa kuvaa sweta kama ilivyoainishwa hapo juu.
e) Wanafunzi wavae sare kamili ya shule wanaposafiri kwenda likizo au wanaporudi kutoka likizo na kila watokapo nje ya shule kwa dharura yoyote.

## 7.3 Nidhamu

a) Hairuhusiwi mwanafunzi kutoka nje ya shule bila ruhusa ya mwalimu wa zamu au Ofisi kuu.
b) Hairuhusiwi mwanafunzi kuzurura nje wakati wa vipindi. Aidha wanafunzi wanaohitaji kujisomea zaidi baada ya ratiba ya masomo wanashauriwa kuwa maktaba, ukumbi au darasa maalum litakalotengwa kama ukumbi wa shule utakuwa na matumizi mengine.
c) Hairuhusiwi kwa wanafunzi kuja na simu za mkononi shuleni wala kutumia simu ambazo hajaidhinishwa.
d) Mwanafunzi haruhusiwi kupiga kelele anapokuwa parade, darasani au bwenini.
e) Mwanafunzi hairuhusiwi kufuga kucha, nywele na unyoaji wa vipara hauruhusiwi.
f) Wanafunzi wawapo shuleni, matibabu yao yatafanyika katika hospitali za umma.
g) Mwanafunzi awapo shuleni hatoruhusiwa kutoka nje ya shule isipokuwa siku maalumu (outing day na kwa ruhusa maalumu).
h) Kila mwanafunzi lazima ajue kuimba kwa ufasaha nyimbo zifuatazo:
    - Wimbo wa "Taifa"
    - Wimbo wa "Tanzania nakupenda"
    - Wimbo wa "Shule".
    - Wimbo wa "Tazama ramani"
    - Wimbo wa "Kuwasha mwenge"
    - "Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki"

## 7.4 Sehemu ambazo wanafunzi hawaruhusiwi kufika bila kibali

- Chumba cha walimu (Staff room)
- Maabara
- Ofisi za Walimu
- Jikoni
- Nyumba za walimu na wafanyakazi

## 7.5 Sehemu zilizopigwa marufuku wanafunzi kutembelea.

- Vilabu vya pombe
- Majumba ya starehe (Clubs)
- Nyumba za kulala wageni.

## 7.6 Makosa yatakayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule.

Makosa yaliyoorodheshwa hapa chini yanasababisha mwanafunzi kufukuzwa shule moja kwa moja.

a) Kumiliki, kukutwa au kutumia kadi ya simu au simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

b) Wizi.
c) Kutohudhuria shule masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
d) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
e) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
f) Kupigana wanafunzi kwa wanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote.
g) Kufuga ndevu.
h) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
i) Uvutaji wa sigara na bangi.
j) Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa.
k) Kushiriki matendo ya uhalifu na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
l) Ushabiki wa Siasa, dini na ukabila haviruhusiwi.
m) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
n) Kudharau Bendera na wimbo wa Taifa
o) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
p) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi ikiwemo kuchora/kuandika ukuta, kuharibu mabomba, viti au meza.
q) Kukataa adhabu kwa kudharau au kwa kiburi
r) Kukutwa nje ya shule bila ruhusa au kibali (Utoro)

*******************KARIBU SHULE YA SEKONDARI BIHAWANA****************

*Mwl. Liberatus L. Ntilema*

**MKUU WA SHULE**

# <u>Fomu Na. 1</u>
# AHADI YA MZAZI / MLEZI

Mimi________________________wa S.L.P______Mji__________Simu ______________ na mwenye picha hapo juu. Ambaye kazi yangu ni _______________natamka hapa kama mzazi / mlezi wa ____________________. Ninakubali kwa hiari yangu mwanangu asome katika Shule ya Sekondari Bihawana kuanzia tarehe __________________. Ninaahidi kama ifuatavyo:-

1. Kwamba nimekubali chaguo alilopewa mwanangu na sitamruhusu kubadilisha hadi apate kibali cha maandishi kutoka kwa mamlaka husika.
2. Ninaahidi kumpatia mwanangu vifaa vyote kama vilivyoainishwa katika fomu ya kujiunga ikiwemo SARE KAMILI ya shule bila kuharibu chochote.
3. Ninatambua ya kuwa walimu wanahitaji ushirikiano wangu katika kumpatia mwanangu elimu na nitashirikiana nao bega kwa bega kwa masuala yanayomuhusu mwanangu kitaaluma na nidhamu ili aweze kufikia malengo yake na ya Taifa.
4. Naahidi kuwa endapo mwanangu ataenda kinyume na taratibu zilizoainishwa katika fomu hii achukuliwe hatua stahili za kinidhamu kama alivyoorodheshewa.

Jina:___________________________ saini_________________

Tarehe:______________ Uhusiano na mwanafunzi:_____________

# Fomu Na. 2
# AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi mwanafunzi ________________________________Wa kidato cha Tano chaguo______________(tahasusi) mwaka wa masomo 2022/2023. Ninakiri kusoma, kuelewa na kuahidi kutii taratibu zote zilizoainishwa katila fomu iliyotumwa kwangu na Mkuu wa shule ya Sekondari Bihawana. Nitatoa ushirikiano wa kutosha kwa walimu wangu na shule kwa ujumla katika muda wangu wote nitakaokuwa shuleni ili niweze kupata elimu na kuendeleza jamii na Taifa langu.

Jina:_____________________________ Saini_______________

Tarehe: ___________________

# Fomu Na. 3
# KIAPO CHA MZAZI / MLEZI

Mimi:______________________wa S.L.P___________Mji___________ Simu Na_____________. Nakiri kukaa na kuzungumza na mwanangu juu ya taratibu na sheria za shule na ninaahidi kumsaidia na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Mkuu wa Shule na walimu kwa muda wote ambao mwanangu atakapokuwa katika shule hii. Ninatambua madhara ya mwanangu kutembelewa na wageni wasioeleweka wakati akiwa shuleni na ninaomba shule iwatambue watu watatu (3) ambao wanahusika katika muda wote ambao atakuwa shuleni nao ni:-(ambatanisha picha passport size zao)

*Picha ya ndugu wa Kwanza*

Jina:______________________________ Kazi:_____________
Makazi: __________________ Simu: ____________________
Uhusiano na mwanafunzi:___________________________________

*Picha ya ndugu wa Pili*

Jina:______________________________ Kazi:_____________
Makazi: __________________ Simu: ____________________
Uhusiano na mwanafunzi:___________________________________

*Picha ya ndugu wa Tatu*

Jina:______________________________ Kazi:_____________
Makazi: __________________ Simu: ____________________
Uhusiano na mwanafunzi:___________________________________

Saini ya mzazi/ mlezi: _______________________ Tarehe: ________________

# Fomu Na. 4

# UTHIBITISHO WA AFYA

Bihawana Secondary school
P.O. BOX 934,
DODOMA.

Student's photo

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

To be completed by Medical Officer from a known Public Hospital or Health Centre in respect to all entrants

Full name…………………….................Age……...Sex…………year…..

1. Blood count (Red and White) ……………………………………...
2. Urinalysis Test ………………………………………………………….
3. Syphilis test………………………………………………………………
4. T.B.…………………………………………………………………………
5. Eye Test ……………………………………………………………………
6. Ears…………………………………………………………………………
7. Spleen………………………………………………………………………
8. Abdomen ………………………………………………………………….

ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical impairment, family disease, chronic infections etc.

……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

I certify that the above named individual is fit to pursue studies as stated above

………………………………..          …………………………………….
Name and Designation          Signature and Official stamp

………………………………..          …………………………………
STATION          DATE

**NOTE:**

1. *Medical officer during the course of this Examination please attend the individual according to any diagnosed case.*
2. *The dully filled form must be handed to the Head of the School during registration week, under No circumstances should a student be registered without certification of his/her physical fitness.*